04

Office of Chief Government Statistician

Police Headquarter Zanzibar

# OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR KWA MWEZI WA APRILI, 2023

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA APRILI 2023

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 148 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Aprili, 2023 ambapo waathirika walikuwa 152. Wengi wao walikuwa watoto sawa na asilimia 85.5,wanawake asilimia 10.5 na wanaume asilimia 4.0, miongoni mwa watoto wasichana walikuwa 99 (asilimia 76.2) na wavulana walikuwa 31 (asilimia 23.8).


**Kielelezo 1.1 Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Aprili 2023**





**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 37) sawa na asilimia 25.0 kwa kila wilaya, ikifuatia wilaya ya Magharibi "A" ambapo imeripotiwa matukio 35 (asilimia 23.6). Ambapo wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote ambapo matukio matatu (3) sawa na asilimia 2.0.

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Aprili 2023**




**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**




Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 4.5 kutoka matukio 155 kwa mwezi wa Machi, 2023 hadi 148 mwezi wa Aprili, 2023. Aidha, Wilaya ya Mjini iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Machi 2023 (matukio 43) ambapo pia Mjini imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Aprili 2023 (matukio 37). Wilaya ya ya Kusini iliripotiwa matukio mawili (2) kwa mwezi wa Machi 2023. Hatahivyo, wilaya ya Kusini imeripotiwa matukio matatu (3) kwa mwezi wa Aprili 2023.

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Machi 2023 na Mwezi wa Aprili 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Machi 2023 | Aprili 2023 | Machi 2023 | Aprili 2023 | Machi 2023 | Aprili 2023 | Machi 2023 | Aprili 2023 | Machi 2023 | Aprili 2023 | Machi 2023 | Aprili 2023 | Machi 2023 | Aprili 2023 |
| Kaskazini 'A' | 6 | 4 | 5 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 10 | 1 | 6 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Kati | 7 | 9 | 4 | 4 | 2 | 0 | 1 | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 43 | 37 | 19 | 14 | 8 | 7 | 0 | 0 | 2 | 1 | 2 | 3 | 12 | 12 |
| Magharibi 'A' | 34 | 35 | 14 | 19 | 8 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 4 | 7 | 10 |
| Magharibi 'B' | 36 | 26 | 17 | 13 | 5 | 4 | 2 | 0 | 2 | 1 | 1 | 1 | 9 | 7 |
| Wete | 12 | 6 | 3 | 3 | 2 | 2 | 0 | 1 | 3 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 6 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 4 | 8 | 1 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 4 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **155** | **148** | **69** | **72** | **29** | **20** | **6** | **4** | **8** | **4** | **14** | **16** | **29** | **32** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar**

Idadi ya matukio kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 117.6 kutoka matukio 68 kwa mwezi wa Aprili, 2022 hadi 148 mwezi wa Aprili, 2023. Aidha, Wilaya ya Magharibi "B" iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Aprili 2022 (matukio 19) ambapo Wilaya ya Mjini imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Aprili 2023 (matukio 37).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Aprili 2022 na Aprili 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 4 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 10 | 3 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Kati | 4 | 9 | 3 | 4 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 3 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 15 | 37 | 3 | 14 | 2 | 7 | 7 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 2 | 12 |
| Magharibi 'A' | 9 | 35 | 4 | 19 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 | 3 | 10 |
| Magharibi 'B' | 19 | 26 | 6 | 13 | 2 | 4 | 3 | 0 | 1 | 1 | 3 | 1 | 4 | 7 |
| Wete | 6 | 6 | 3 | 3 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 6 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 6 | 8 | 2 | 4 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **68** | **148** | **28** | **72** | **9** | **20** | **12** | **4** | **1** | **4** | **8** | **16** | **10** | **32** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar**

Miongoni mwa watoto 130 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 69, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 19, wasichana walioingilia kinyume na maumbile ni 3, Kutorosha walikuwa wasichana 4 , shambulio la aibu walikuwa 15 ambapo wasichana walikuwa 14 na mvulana mmoja (1) na shambulio walikuwa 20 ambapo wasichana walikuwa 9 na wavulana walikuwa 11.

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Aprili 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 6 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 8 | 3 | 0 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 29 | 12 | 6 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 4 | 4 |
| Magharibi 'A' | 31 | 18 | 2 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 3 | 4 |
| Magharibi 'B' | 21 | 12 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 |
| Wete | 5 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 6 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 12 | 6 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **130** | **69** | **19** | **3** | **4** | **0** | **14** | **1** | **9** | **11** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar**

Miongoni mwa wanawake 16 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa ni watano (5), kuingilia kinyume na maumbile alikuwa mwanamke mmoja (1),, shambulio la aibu walikuwa wanawake wawili (2) na shambulio walikuwa wanawake nane(8).

**Jadweli 1.4a: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya, Aprili 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Kati | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 5 | 2 | 0 | 0 | 1 | 2 |
| Magharibi 'A' | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Wete | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **16** | **5** | **1** | **0** | **2** | **8** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar**

**Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya, Aprili 2023**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **6** | **2** | **0** | **0** | **4** |


**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar**

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 61) sawa na asilimia 46.9 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 33) sawa na asilimia 25.4. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17(matukio 40) sawa na asilimia 58.0 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

## Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Aprili 2023

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume namaumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 7 | 4 | | | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 15 |
| 6-10 | | 2 | 8 | | | 0 | 0 | 1 | 0 | 6 | 3 | 1 | 21 |
| 11-14 | | 20 | 4 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 4 | 33 |
| 15-17 | | 40 | 3 | | | 2 | 0 | 3 | 0 | 5 | 4 | 4 | 61 |
| **Jumla** | | 69 | 19 | | | 3 | 0 | 4 | 1 | 14 | 11 | 9 | 130 |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**



Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Aprili, 2023 yamepungua kwa asilimia 3.0 (matukio 130) ukilinganisha na mwezi wa Machi, 2023 (matukio 134). Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15- 17 kwa mwezi uliopita imepungua kwa asilimia 10.3 kutoka matukio 68 kwa mwezi Machi 2023 hadi matukio 61 kwa mwezi wa Aprili 2023.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Machi 2023 na Aprili 2023**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Machi 2022 | Jumla Aprili 2023 |
| | Machi 2022 | Aprili 2023 | Machi 2022 | Aprili 2023 | Machi 2022 | Aprili 2023 | Machi 2022 | Aprili 2023 | Machi 2022 | Aprili 2023 | Machi 2022 | Aprili 2023 | | |
| 0-5 | 1 | 7 | 2 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 5 | 15 |
| 6-10 | 5 | 2 | 16 | 8 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 6 | 5 | 4 | 29 | 21 |
| 11-14 | 10 | 20 | 8 | 4 | 2 | 0 | 1 | 0 | 3 | 1 | 8 | 8 | 32 | 33 |
| 15-17 | 49 | 40 | 2 | 3 | 1 | 2 | 5 | 3 | 6 | 5 | 5 | 8 | 68 | 61 |
| **Jumla** | **65** | **69** | **28** | **19** | **5** | **3** | **6** | **4** | **12** | **15** | **18** | **20** | **134** | **130** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwa mwaka uliopita yameongezeka kutoka matukio 60 kwa mwezi wa Aprili, 2022 hadi matukio 130 kwa mwezi wa Aprili, 2023, ambapo idadi ya matukio katika umri wa miaka yote yameongezeka kwa mwezi wa Aprili 2023 isipokuwa umri wa miaka 6-10.


**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Aprili 2022 na Aprili 2023**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Aprili 2022 | Jumla Aprili 2023 |
| | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | Aprili 2022 | Aprili 2023 | | |
| 0-5 | 0 | 7 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 | 2 | 15 |
| 6-10 | 4 | 2 | 6 | 8 | 9 | 0 | 0 | 1 | 3 | 6 | 0 | 4 | 22 | 21 |
| 11-14 | 6 | 20 | 3 | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 8 | 12 | 33 |
| 15-17 | 15 | 40 | 0 | 3 | 2 | 2 | 1 | 3 | 0 | 5 | 6 | 8 | 24 | 61 |
| **Jumla** | **25** | **69** | **9** | **19** | **13** | **3** | **1** | **4** | **6** | **15** | **6** | **20** | **60** | **130** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Matukio mengi zaidi yanaonesha kutokea nyumbani kwa mtuhumiwa (matukio 62) sawa na asilimia 40.8 ukilinganisha na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea, Aprili 2023**




**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Matukio 114 kati ya matukio 148 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Polisi  sawa na asilimia 77.0, matukio 30 yapo Ofisi ya Mashtaka sawa na asilimia 20.2, matukio mawili (2) yapo mahakamani sawa na asilimia 1.4 na matukio mawili (2) limefungwa na polisi sawa na asilimia  1.4.


**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa, Aprili 2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwanamme | Wanawake | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 74 | | 5 | 69 | | 0 | 0 | 0 | 2 | 20 | 50 |
| Kulawiti | 20 | 2 | | | 19 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 15 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 4 | | 1 | 3 | | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Kutorosha | 4 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 16 | 0 | 2 | 14 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 15 |
| Shambulio | 32 | 4 | 8 | 9 | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 27 |
| **Jumla** | **148** | **6** | **16** | **99** | **31** | **2** | **0** | **0** | **2** | **30** | **114** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Aprili 2023 ni 148 kati yao 118 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 79.7  kati ya watuhumiwa wote walioripotiwa.

**Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia, Aprili 2023**




**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 148 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Aprili, 2023 ambapo wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 37) sawa na asilimia 25.0. Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 4.5 kutoka matukio 155 kwa mwezi wa Machi, 2023 hadi 148 mwezi wa Aprili, 2023.

Matukio 114 kati ya matukio 148 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Polisi sawa na asilimia 77.0, matukio 30 yapo Ofisi ya Mashtaka sawa na asilimia 20.2, matukio mawili (2) yapo mahakamani sawa na asilimia 1.4 na matukio mawili (2) limefungwa na polisi sawa na asilimia 1.4.

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Aprili 2023**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 3 | | 3 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 6 | 4 | 10 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 27 | | 27 | | 7 | 7 | 4 | | 4 | 2 | 0 | 2 | 6 | 1 | 7 | 7 | 8 | 15 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 5 | | 5 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu za kazi | 1 | | 1 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/ Madrasa | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 11 | | 11 | | 4 | 4 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 27 | | 27 | | 10 | 10 | 0 | | 0 | 1 | 0 | 1 | 6 | 0 | 6 | 4 | 3 | 7 |
| **Jumla** | **74** | | **74** | | **21** | **21** | 4 | | **4** | **4** | **0** | **4** | **16** | **1** | **17** | **17** | **15** | **32** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Jadweli 1.12: Mlinganisho wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio kwa mwezi Machi 2023 na Aprili 2023**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyumena maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Machi 2023 | Jumla Aprili 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Machi | Aprili | Machi | Aprili | Machi | Aprili | Machi | Aprili | Machi | Aprili | Machi | Aprili | | |
| Nyumbani kwa Muathirika | 6 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 | 2 | 6 | 10 | 18 | 16 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 26 | 27 | 11 | 7 | 2 | 4 | 4 | 2 | 5 | 7 | 5 | 15 | 53 | 62 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 9 | 5 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 6 | 0 | 21 | 5 |
| Sehemu za kazi | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 6 | 1 |
| Skuli/ Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 9 | 11 | 4 | 4 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 17 | 17 |
| Sehemu nyengine(Vichakanina kwengine) | 19 | 27 | 9 | 10 | 0 | 0 | 2 | 1 | 4 | 6 | 6 | 7 | 40 | 51 |
| **Jumla** | **69** | **74** | **29** | **21** | **6** | **4** | **8** | **4** | **14** | **17** | **29** | **32** | **155** | **152** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Jadweli 2.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Aprili 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 10 | 6 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Kati | 9 | 4 | 0 | 3 | 1 | 1 | 0 |
| Kusini | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 37 | 14 | 7 | 0 | 1 | 3 | 12 |
| Magharibi 'A' | 35 | 19 | 2 | 0 | 0 | 4 | 10 |
| Magharibi 'B' | 26 | 13 | 4 | 0 | 1 | 1 | 7 |
| Wete | 6 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 6 | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Chake Chake | 8 | 4 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Mkoani | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **148** | **72** | **20** | **4** | **4** | **16** | **32** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Machi 2023 na Aprili 2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Machi | Aprili | Machi | Aprili | Machi | Aprili | Machi | Aprili | Machi | Aprili |
| Kubaka | 69 | 72 | 4 | 5 | 65 | 69 | [redacted] | | | |
| Kulawiti | 29 | 20 | [redacted] | | | | 28 | 19 | 1 | 2 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | 4 | 1 | 1 | 5 | 3 | [redacted] | | | |
| Kutorosha | 8 | 4 | 2 | 0 | 6 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 14 | 16 | 2 | 2 | 11 | 14 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio | 29 | 32 | 5 | 8 | 9 | 9 | 9 | 11 | 6 | 4 |
| **Jumla** | **155** | **148** | **14** | **16** | **96** | **99** | **38** | **31** | **7** | **6** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Aprili 2022 na Aprili 2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Aprili | Aprili | Aprili | Aprili | Aprili | Aprili | Aprili | Aprili | Aprili | Aprili |
| Kubaka | 28 | 72 | 3 | 5 | 25 | 69 | [redacted] | [redacted] | [redacted] | [redacted] |
| Kulawiti | 9 | 20 | [redacted] | [redacted] | [redacted] | [redacted] | 9 | 19 | 0 | 2 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 12 | 4 | 0 | 1 | 13 | 3 | [redacted] | [redacted] | [redacted] | [redacted] |
| Kutorosha | 1 | 4 | 0 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 8 | 16 | 2 | 2 | 6 | 14 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio | 10 | 32 | 4 | 8 | 3 | 9 | 3 | 11 | 0 | 4 |
| **Jumla** | **68** | **148** | **9** | **16** | **48** | **99** | **12** | **31** | **0** | **6** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Jadweli 5.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea Aprili 2023**

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajis | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 6 | 5 | 0 | 0 | 1 | 2 | 14 |
| 03:01 - 6:00 Mchana | 13 | 3 | 1 | 1 | 4 | 3 | 25 |
| 6:01 - 9:00 Jioni | 7 | 4 | 1 | 0 | 1 | 8 | 21 |
| 9:01 - 1200 Jioni | 9 | 1 | 1 | 2 | 5 | 7 | 25 |
| 12:01 - 3:00 usiku | 23 | 5 | 0 | 1 | 6 | 7 | 42 |
| 3:01 - 6:00 Usiku | 10 | 3 | 1 | 0 | 0 | 3 | 17 |
| 6:01 - 09:00 Usiku | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 6 |
| **Jumla** | **74** | **21** | **4** | **4** | **17** | **32** | **152** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Zingatia Maelezo**

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004.

Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**


OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua,2321, MMP, Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237, MMP, Barua
pepe:cidphqznz@gmail.com Nukushi:
024223136